

Idara ya Afya ya Vermont Dozi ya Pili ya Chanjo ya COVID-19 Fomu ya Idhini

Jina la Mgonjwa: _____
Tarehe ya Kuzaliwa: _____

Imechapishwa na Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC):

Matumizi sawa ya aina tofauti za chanjo ya COVID-19

Chanjo yoyote iliyoidhinishwa sasa ya COVID-19 ya FDA inaweza kutumika ifaavyo; ACIP haipendelei aina yoyote ile. Walakini, chanjo za COVID-19 **haziwezi** kubadilishana matumizi. Usalama na ufanisi wa msururu wa mchanganyiko wa bidhaa haujatathminiwa. Dozi zote za msururu zinapaswa kutumika na aina sawa.

Katika hali za kipekee ambapo aina za chanjo ya mRNA zilizotolewa kwa dozi ya kwanza haiwezi kubainishwa au haipatikani tena, chanjo yoyote inayopatikana ya mRNA ya COVID-19 inaweza kutolewa kwa muda wa chini ya siku 28 kati ya dozi ili kukamilisha msururu wa chanjo ya mRNA ya COVID-19. Katika hali ambapo aina hiyo ya chanjo ya mRNA haipatikani kwa muda, ni vyema kuchelewesha dozi ya pili (hadi wiki 6) kupokea aina hiyo kuliko kupokea msururu wa mchanganyiko kwa kutumia aina tofauti. Ikiwa dozi mbili za aina tofauti za chanjo ya mRNA ya COVID-19 zinatolewa katika hali hizi (au bila kukusudia), hakuna dozi ya ziada ya aina yoyote inayopendekezwa kwa wakati huu. Watu kama hao wanazingatiwa kuwa wamepewa chanjo kamili dhidi ya COVID-19 \geq wiki 2 baada ya kupokea dozi ya pili ya chanjo ya mRNA.

Usalama na ufanisi wa chanjo ya Janssen ya COVID-19 inayotolewa baada ya chanjo ya mRNA ya COVID-19 haujabainishwa. Walakini, katika hali zingine, za kipekee ambapo mgonjwa alipokea dozi ya kwanza ya chanjo ya mRNA ya COVID-19 lakini hawezi kumaliza msururu na chanjo sawa au tofauti ya mRNA ya COVID-19 (kwa mfano, kwa sababu ya madhara), dozi moja ya Chanjo ya Janssen ya COVID-19 inaweza kuzingatiwa kwa muda wa chini ya siku 28 kutoka kwa dozi ya chanjo ya mRNA ya COVID-19. Wagonjwa wanaopokea chanjo ya Janssen ya COVID-19 baada ya dozi ya chanjo ya mRNA ya COVID-19 wanapaswa kuchukuliwa kwamba wamepokea chanjo halali, ya dozi moja ya Janssen—sio msururu wa mchanganyiko waa chanjo—na wanachukuliwa kuwa wamepewa chanjo kamili dhidi ya COVID-19 \geq wiki 2 baada ya kupokea dozi moja ya chanjo ya Janssen.

- **Nimewaarifu wafanyakazi wa kliniki juu ya kile ninachoamini kuwa aina ya chanjo ya kweli na sahihi ya COVID-19 mimi (au mgonjwa hapo juu) nilipokea kama dozi ya kwanza (yaani Pfizer-BioNTech, Moderna).**
- **Nimewaarifu wafanyakazi wa kliniki kile ninaamini kuwa ni tarehe ya kweli na sahihi ambayo mimi (au mgonjwa hapo juu) nilipokea dozi ya kwanza ya chanjo ya COVID-19.**

**Idara ya Afya ya Vermont
Dozi ya Pili ya Chanjo ya COVID-19
Fomu ya Idhini**

- Ninaelewa kuwa Idara ya Afya ya Vermont na kliniki hii ya chanjo haziwezi kuthibitisha usahihi wa dozi yangu ya kwanza (au ya mgonjwa aliyetajwa hapo juu) (yaani Pfizer-BioNTech, Moderna).
- Nimesoma nyenzo zilizo hapo juu kutoka kwa Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) kuhusu ubadilishaji wa aina ya chanjo ya COVID-19 zinazozungumzia kubadilisha aina ya chanjo iliyopokelewa kwa dozi ya pili.
- Ninaelewa kuwa usalama na ufanisi wa kupokea aina mbili tofauti za chanjo ya COVID-19 (kwa mfano kupokea Moderna katika dozi ya kwanza na Pfizer-BioNTech kama dozi ya pili) haujatafitiwa na kubainishwa.

Saini ya Mgonjwa: _____

Tarehe ya Kusainiwa kwa Fomu ya Idhini:

Saini ya Mzazi au Mlezi Halali* (iwapo mgonjwa ni wa umri wa chini ya miaka 18)

*Ikiwa mtoto yuko chini ya ulinzi wa serikali, saini ya mwakilishi aliyeidhinishwa inahitajika.

Jina la Mzazi/Mlezi Halali (tafadhali andika): _____

Nambari ya simu ya Mchana ya Mzazi/Mlezi:** _____

** Ikiwa mzazi/mlezi halali hatakuwepo kwenye kliniki.